

Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe 2023: Hatua Muhimu za Kujenga Nyumba Zaidi, Kusaidia Tabaka La Kati La Kiuchumi, na Kufanya Maisha Kuwa Nafuu Zaidi

Hatua muhimu zilizoainishwa kwenye Taarifa ya Kiuchumi ya Majira ya Kipupwe 2023 ni pamoja na:

Mpango wa Ujenzi wa Makazi wa Canada

- Mfuko wa Kuongeza Kasi ya Ujenzi wa Nyumba wa dola bilioni 4, ambao unasaidia kupunguza urasimu na kujenga zaidi ya nyumba mpya 100,000 kote nchini Canada, kwa haraka zaidi;
- [Kubadilisha matumizi zaidi ya ardhi ya serikali kuu ili kujenga nyumba juu yake](#);
- Kuondoa kodi ya GST kwenye ujenzi mpya wa nyumba za kupangisha, ikiwa ni pamoja na mashirika ya ushirika yanayotoa huduma za upangishaji wa muda mrefu;
- [Kuwezesha upatikanaji wa dola bilioni 20 katika ufadhili wa gharama nafuu kwa ujenzi wa nyumba za kupangisha](#) ili kujenga hadi nyumba 30,000 zaidi kwa mwaka;
- Kufadhili nyumba zaidi za kupangisha kwa kutoa dola bilioni 15 kama mikopo kupitia Programu ya Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba za Gorofa, ili kusaidia ujezi wa nyumba mpya 30,000;
- Kujenga nyumba nafuu zaidi kwa watu nchini Canada walio hatarini zaidi kwa kutumia dola bilioni 1 kwa Mfuko wa Makazi Nafuu, ili kusaidia kujenga zaidi ya nyumba mpya 7,000;
- Kuondoa vikwazo vya uhamaji wa kazi ndani ya Canada, kwa kutoa kipaumbele kwa wafanyakazi wa ujenzi na wataalamu wa afya, na kuweka kipaumbele kwa mafundi stadi kwa kuwapatia makazi ya kudumu nchini (permanent residency) ;
- Kukabiliana na upangishaji wa muda mfupi usiozingatia sheria na kusaidia utekelezwaji wa sheria dhidi ya upangishaji wa muda mfupi katika manispaa za miji mbalimbali na;
- Mkataba Mpya wa Mikopo ya Nyumba wa Canada (Canadian Mortgage Charter) ili kuhakikisha watu wa nchini Canada walio hatarini kifedha wanapata unafuu wa mikopo ya nyumba wanayoweza kutarajia kutoka benki zao ili kuwasaidia kulipa na kubakia katika nyumba zao.

Kusaidia Tabaka la Kati La Kiuchumi Lililo Imara Zaidi

- [Kuimarisha ushindani nchini Canada](#), kitu ambacho kinamaanisha bei za chini na chaguo zaidi, kwa kurekebisha sheria ili kukabiliana na mienendo isiyo ya haki inayopandisha gharama;

- Kuhakikisha makampuni makubwa matano ya vyakula nchini Canada yanatimiza ahadi zao za kutengamisha bei, na [kuongeza ushindani katika sekta ya vyakula](#);
- Kuondoa kodi ya GST kwa huduma za saikotherapia na ushauri nasaha, ili kufanya huduma za afya ya akili kuwa nafuu zaidi kwa watu nchini Canada;
- Kuendelea kukabiliana na ada zisizo za lazima, ikiwa ni pamoja na [kupunguza ada za fedha zisizotosha kwenye akaunti \(NSF\) zinazotozwa na benki](#), kuchunguza viwango vya kutumia simu nje ya nchi, na kuhakikisha kuwa mashirika ya ndege yanawapa mahali pa kukaa watoto wote walio chini ya umri wa miaka 14 karibu na watu wazima wanaosafiri pamoja nao bila gharama za ziada;
- Kubadilisha sheria ili kuunga mkono haki za watu nchini Canada kutengeneza vifaa na bidhaa zao kwa kuzuia wazalishaji kukataa kutoa njia za kutengeneza kwa njia au namna inayozuia ushindani;
- Kujiunga na faida mpya ya Bima ya Ajira (Employment Insurance) ambayo itatoa wiki 15 za faida zinazoweza kutumiwa kwa pamoja miongoni mwa wazazi; na,
- [Kuimarisha akaunti za benki za gharama nafuu na za bila gharama](#) kuakisi hali halisi ya benki za kisasa huku ikitaja Mchunguzi Maalum (Ombudsman) huru mmoja kusaidia watu nchini Canada kutatua malalamiko dhidi ya benki zao.